**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**

# MUHTASARI WA MAFUNZO YA UALIMU NGAZI YA CHETI ELIMU YA MSINGI

# HAIBA NA MICHEZO

**2009**

© Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi 2009

ISBN..........................................................

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kutafsiri, kunakili, kupiga chapa muhtasari huu kwa namna yoyote ile bila idhini ya Taasisi ya Elimu Tanzania.

Umetayarishwa na:
Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P. 35094
Dar-es-Salaam.
Tanzania

Simu: +255 222 773006, 2774420
Faksi: +255 222 774420
Barua pepe: director.tie @tie.go.tz

## IDHINI

Mafunzo ya Ualimu wa Elimu ya Msingi Ngazi ya Cheti ni ya miaka miwili na yamekusudiwa kuandaa walimu mahiri wenye uwezo wa kufanya kazi kwa dhati. Walimu hao watafundisha katika shule za msingi. Mwalimu mwanafunzi atatambuliwa kuwa ni mwalimu baada ya kuhudhuria na kufaulu mafunzo ya cheti ya miaka miwili ambamo pia atafanya na kufaulu mazoezi ya kufundisha.

Andiko hili linaidhinishwa kuwa ni **Muhtasari wa Haiba na Michezo** wa mwaka 2009.

**Umeidhinishwa na ......................................................**

**Saini...............................................................................**

**Tarehe...................................................................2009**

**Kamishna wa Elimu**
Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi
S.L.P 9121
**Dar -es -Salaam**

Simu: +255 222 110150, 110179, 11046
Nukushi: +255 222 113271
Wovuti: www.moe.go.tz

## YALIYOMO

UTANGULIZI ........................................................................................ iv
Sababu za Kuwa na Muhtasari Huu ........................................................................ iv
Madhumuni ya Somo la Haiba na Michezo ........................................................... iv
Ujuzi wa Somo la Haiba na Michezo .......................................................................v
Malengo ya Somo la Haiba na Michezo ..................................................................v
Muundo wa Muhtasari ............................................................................................ vi
Muda wa Mafunzo ................................................................................................. vi
Upimaji na Tathmini wa Somo ............................................................................... vi
Jedwali la Upimaji Endelezi ................................................................................... vii
1.0 MISINGI YA UFUNDISHAJI WA SOMO LA HAIBA NA MICHEZO .1
1.1 Dhana ya Misingi ya Ufundishaji .........................................................1
1.2 Ufundishaji kwa Kutumia Misingi .......................................................2
2.0 MAANDALIZI YA MAANDIKO, VIFAA NA ZANA ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA .......................................................6
2.1 Uchambuzi wa Muhtasari ....................................................................6
2.2 Uchambuzi wa Vitabu vya Kiada ........................................................7
2.3 Uchambuzi wa Machapisho ya Ziada ...................................................7
2.4 Uchambuzi wa Kiongozi cha Mwalimu ...............................................8
3.0 ZANA ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA ....................................10
3.1 Aina za Zana .......................................................................................10
3.2 Upatikanaji wa Zana ...........................................................................10
3.3 Matumizi na utunzaji wa zana za kufundishia na kujifunzia .............11
4.0 MAANDALIZI YA UFUNDISHAJI WA SOMO LA HAIBA NA MICHEZO .........................................................................................13
4.1 Uandaaji wa Azimio la Kazi ...............................................................13
4.2 Andalio la Somo ..................................................................................14
4.4 Nukuu za Somo ...................................................................................15
4.5 Ufundishaji wa Mfano ........................................................................16
5.0 UPIMAJI NA TATHIMINI YA UFUNDISHAJI WA SOMO LA HAIBA NA MICHEZO ..................................................................................19
5.1 Upimaji katika somo la Haiba na Michezo .......................................19
5.2 Zana za Upimaji katika somo la Haiba na Michezo ...........................20
5.3 Tathmini katika somo la Haiba na Michezo ......................................20
Rejea .......................................................................................................................22

## UTANGULIZI

Muhtasari wa somo la Haiba na Michezo umeandaliwa ili kumjengea mwanachuo stadi za kufundisha haiba na michezo katika shule za msingi.
Muhtasari huu umetayarishwa kwa mara ya kwanza

Lengo la kuwa na somo hili ni kuwatayarisha wanachuo kuwa walimu wa shule za msingi na wenye uwezo wa kufundisha somo hilo kwa kujiamini. Mbinu za jinsi ya kulifundisha somo la Haiba na Michezo zimetolewa za kutosha, na mikakati ya jinsi ya kulifundisha pia imefafanuliwa. Muhtasari huu umezingatia pia masuala mtambuko ambayo ni Elimu Jumuishi, Ukimwi, mazingira, Haki za watoto na Elimu ya jinsia.

## Sababu za Kuwa na Muhtasari Huu

Kuanzishwa kwa muhtasari huu unatokana na uamuzi wa serikali wa mwaka 2007 wa kuimarisha mafunzo ya ualimu katika nyanja ya michezo pamoja na uamuzi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi 2008 wa kuimarisha mafunzo ya ualimu na kutatua tatizo la upungufu wa walimu ngazi ya cheti linalokabili nchi kwa ujumla. Hii ni pamoja na kukidhi mahitaji na idadi ya walimu wa michezo kutokana na kupanuka kwa sekta ya elimu ya msingi kufuatia kutekelezwa kwa mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM), kuongezeka kwa mahitaji ya walimu wenye kiwango cha juu cha taaluma ya michezo na utaalam na kushughulikia masuala mtambuko.
Muhtasari huu umeandaliwa kumwezesha mwanachuo kupata maarifa na ujuzi wa katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo.

## Madhumuni ya Somo la Haiba na Michezo

Madhumuni ya somo la Haiba na Michezo ni:

a) Kukuza kiwango cha maarifa cha mwanachuo na uwezo wao wa kutumia njia shirikishi na ufundishaji unaojenga maana katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo.

b) Kuwawezesha wanachuo kujenga stadi za uchezaji wa michezo mbalimbali na ujezi wa stadi hizo kwa wanafunzi.
c) Kuandaa wanachuo kujijengea stadi na maarifa ya kushughulikia masuala mtambuka na wanafunzi wenye mahitaji maalumu kwenye somo.

.

**Ujuzi wa Somo la Haiba na Michezo**

Baada ya kusoma mada za somo hili, mwanachuo ataweza kuonesha uwezo wa:

a) Kutumia mbinu za michezo kwa ufanisi katika ufundishaji utakaomwezesha wanafunzi wake kujifunza.
b) Kutumia mbinu sahihi za michezo katika ufundishaji na ujifunzaji.
c) Kutumia maarifa, stadi, na mielekeo katika kushughulikia maswala mtambuko.
d) Kupima na kutathmini ufundishaji na ujifunzaji wa somo
e) Kuandaa, kuchambua na kutumia vifaa na zana za kufundishia na kujifunzia kwa ufanisi.
f) Kutumia mazingira katika ufundishaji wa somo la Haiba na Michezo
g) Kuendesha tafiti ndogo za kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa somo hili.

**Malengo ya Somo la Haiba na Michezo**

Baada ya kujifunza kwa miaka miwili, mwanachuo aweze**:**

a) Kubuni, kufaragua, kutengeneza, kutumia zana/vifaa. mbalimbali katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo.
b) Kushirikisha wanafunzi wenye mahitaji mbalimbali katika mchakato wa kufundisha na kujifunza.
c) Kutambua na kutatua matatizo mbalimbali ya wanafunzi katika kufundisha.

d) Kuchopeka masuala mtambuko wakati wa kufundisha mada mbalimbali za somo la Haiba na Michezo
e) Kutumia tafiti ndogo kuboresha ufundishaji wa ujifunzaji.
f) Kupima na kutathmini maarifa, ujuzi na mchakato wa kufundisha somo la Haiba na Michezo.

**Muundo wa Muhtasari**

Muhtasari huu umegawanyika katika sehemu kuu mbili; Sehemu ya kwanza ni utangulizi unaotoa taarifa za awali kuhusiana na somo; sehemu ya pili ni maudhui ya ufundishaji. Maudhui ya Ufundishaji yamegawanyika katika mada, mada ndogo, kila mada ndogo ina lengo mahususi au malengo mahsusi, muda, mbinu za kufundishia na kujifunzia, vifaa/zana na upimaji. Maudhui ya Ufundishaji yana lengo la kumwandaa mwanachuo kupata mbinu mbalimbali za ufundishaji wa somo Haiba na Michezo.

**Muda wa Mafunzo**

Mafunzo ya ualimu ngazi ya cheti ni miaka 2. Somo la Haiba na Michezo lina vipindi viwili kwa wiki, na muda wa kila kipindi ni saa moja (dakika 60). Mkufunzi anapaswa azingatie muda uliopangwa ili kuhakikisha wanachuo wamejifunza mada zote.

**Upimaji na Tathmini wa Somo**

Muhtasari una sehemu ya upimaji ambayo inaonesha jinsi kila lengo mahususi litakavyoweza kupimwa ndani na nje ya darasa. Mkufunzi anashauriwa kutumia mbinu mbalimbali katika kupima maendeleo ya mwanachuo kivitendo. Upimaji utafanyika kwa kutumia zana na mbinu mbalimbali kutegemeana na hali halisi na uwezo wa mwanachuo. Upimaji endelezi ni pamoja na mazoezi ya vitendo, mkoba wa kazi, ufundishaji wa mfano pamoja na ushiriki katika kazi zinazo- tolewa darasani. Upimaji endelezi wa muhtasari huu unabeba jumla ya

alama 20% na wa maudhui alama 30% maudhui yamo katika muhtasari wa Michezo na kufanya jumla ya upimaji endelezi kuwa na 50% na mtihani wa mwisho kubeba alama 50%.

**Jedwali la Upimaji Endelezi**

| S/N | Mbinu za Upimaji | Mrudio | Alama |
|---|---|---|---|
| 1 | Mazoezi ya Vitendo | 3 | 5 |
| 2 | Ufundishaji wa mfano | 3 | 5 |
| 3 | Mkoba wa kazi | 3 | 5 |
| 4 | Mitihani ya Muhula | 3 | 5 |
| **Jumla ya alama za upimaji endelevu** | | | 20 |

## 1.0 MISINGI YA UFUNDISHAJI WA SOMO LA HAIBA NA MICHEZO

### 1.1 Dhana ya Misingi ya Ufundishaji

**Muda: Saa 4**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kueleza umuhimu wa misingi ya kufundishia/kujifunzia somo la Haiba na Michezo.
b) Kufafanua misingi ya kufundishia na kujifunzia somo la Haiba na Michezo.
c) Kutumia misingi katika kufundishia na kujifunzia somo la Haiba na Michezo..

**Mbinu za Kufundishia/kujifunzia**

a) Bungua bongo ,Fikiri, jozisha, shirikisha
b) Majadiliano katika vikundi juu ya matumizi ya misingi ya ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo.

**Vifaa na zana za kujifunzia na kufundishia**

Vitini mbalimbali na muhtasari wa somo la Haiba na Michezo.

**Upimaji**

a) Insha ,jaribio na zoezi
b) Orodha hakiki kuonyesha matumizi ya misingi katika kufundishia na kujifunzia somo la Haiba na Michezo.

## 1.2 Ufundishaji kwa Kutumia Misingi

**Muda :Saa 4**

**Malengo mahususi**

### 1.2.1Utambuzi wa haiba za wanafunzi na uhusiano wake katika kujifunza

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kuainisha haiba mbalimbali za wanafunzi.
b) Kubainisha mbinu za utambuzi wa haiba za wanafunzi
c) Kutumia misingi katika kufundishia na kujifunzia mada za somo.

**Mbinu za Kufundishia/kujifunzia**

a) Bungua bongo, Fikiri, jozisha, shirikisha , majadiliano katika vikundi juu ya matumizi ya misingi ya ufundishaji na ujifunzaji unaozingatia utambuzi wa haiba za wanafunzi na uhusiano wao katika ujifunzaji wa Haiba na Michezo.
b) Onyesho mbinu la ufundishaji.

**Vifaa na zana za kujifunzia na kufundishia**

Vitini mbalimbali na muhtasari wa somo la Haiba na Michezo.

**Upimaji**

a) Insha ,jaribio na zoezi
b) Orodha hakiki kuonyesha matumizi ya misingi katika kufundishia na kujifunzia somo la Haiba na Michezo.

### 1.2.2 Ufundishaji unaolenga kujenga stadi za maisha

**Muda :Saa 4**

**Malengo mahususi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kubainisha za stadi za maisha anazotakiwa kujingewa wanafunzi

b) Ufundishaji unaozingatia stadi za maisha

**Mbinu za Kufundishia/kujifunzia**

a) Bungua bongo ,Fikiri, jozisha, shirikisha
b) Majadiliano katika vikundi juu ya matumizi ya misingi ya ufundishaji na ujifunzaji unaozingatia wa stadi za maisha
c) Onyesho mbinu la ufundishaji.

**Vifaa na zana za kujifunzia na kufundishia**

Vitini mbalimbali na muhtasari wa somo la Haiba na Michezo.

**Upimaji**

Insha ,jaribio na zoezi

Fomu ya uchunguzi na ripoti

**1.2.3 Ufundishaji unaolenga ukuzaji wa stadi binafsi na za timu.**

**Muda :Saa 4**

**Malengo mahususi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

Kuainisha stadi mbalimbali zinazotarajiwa kujengwa katika michezo

Kubainisha mbinu za ujenzi wa stadi za uchezaji.

ufundishaji unaozingatia ujenzi wa stadi za uchezaji

**Mbinu za Kufundishia/kujifunzia**

a) Bungua bongo ,Fikiri, jozisha, shirikisha na kazi za maktaba

b) Majadiliano katika vikundi juu ya matumizi ya misingi ya ufundishaji na ujifunzaji unaozingatia ujenzi wa stadi za uchezaji.
c) Onyesho mbinu la ufundishaji.
d) Vitendo vya uchezaji.

**Vifaa na zana za kujifunzia na kufundishia**

Vitini mbalimbali na muhtasari wa somo la Haiba na Michezo.

**Upimaji**

Insha ,jaribio na zoezi

Fomu ya uchunguzi na ripoti

### 1.2.4 Ufundishaji unaozingatia usalama na utunzaji wa vifaa vya michezo

**Muda :Saa 4**

**Malengo mahususi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kueleza umuhimu wa usalama katika michezo.
b) Kubainisha taratibu za kuzingatia katika ufundishaji wa michezo .
c) Ufundishaji unaozingatia usalama na utunzaji wa vifaa vya michezo.

**Mbinu za Kufundishia/kujifunzia**

a) Kazi binafsi na majadiliano katika vikundi juu ya matumizi ya misingi ya ufundishaji na ujifunzaji unaozingatia usalama na utunzaji wa vifaa
b) Onyesho mbinu la ufundishaji.
c) Vitendo vya uchezaji

**Vifaa na zana za kujifunzia na kufundishia**

Vitini mbalimbali na muhtasari wa somo la Haiba na Michezo.

**Upimaji**

a) Insha ,jaribio na zoezi
b) Fomu ya uchunguzi na ripoti

## 2.0 MAANDALIZI YA MAANDIKO, VIFAA NA ZANA ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA

### 2.1 Uchambuzi wa Muhtasari

**Muda saa: Saa 6**

**Malengo Mahususi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kuchambua vipengele vikuu vya muhtasari wa somo la Haiba na Michezo.
b) Kubainisha mada mbalimbali za muhtasari wa Kiswahili kwa Shule za Msingi.
c) Kuhusianisha vipengele muhimu katika jedwali la muadhui la Muhtasari wa Haiba na Michezo

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Maswali na majibu
b) Kazi za vikundi kuchambua na kuwasilisha juu ya muundo wa muhtasari na uhusiano kati ya vipengele mbalimbali vya muhtasari wa Haiba na Michezo.

**Zana/vifaa vya kufundishia/kujifunzia**

a) Nakala za muhtasari wa somo la Haiba na Michezo kwa shule za msingi.
b) Maswali ya uchambuzi.
c) Moduli ya ufundishaji wa somo la Haiba na Michezo ngazi ya cheti.

**Upimaji**

a) Maswali mafupi, zoezi na kazi binafsi kuchambua vipengele vya Muhtasari.
b) Mkoba wa kazi

## 2.2 Uchambuzi wa Vitabu vya Kiada

Muda: saa 6

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kubainisha sifa za kitabu cha kiada.
b) Kueleza mambo ya kuzingatia katika kutumia kitabu cha kiada.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Kazi za vikundi kujadiliana na kubainisha sifa za kitabu cha kiada cha somo la Haiba na Michezo.
b) Mjadiliano ya vikundi kubaini mambo ya kuzingatia katika kutumia kitabu cha kiada

**Zana/vifaa vya kufundishia/kujifunzia**

a) Vitabu mbalimbali vilivyopitishwa kuwa vya kiada.
b) Maswali ya uchambuzi.
c) Mwongozo wa ufundishaji Haiba na Michezo kwa shule za Msingi

**Upimaji**

a) Maswali ya mdomo kubaini sifa za kitabu cha kiada.
b) Ripoti ya uchambuzi kuonyesha ubora na utoshelevu wa mada kwenye kitabu chochote cha kiada.

## 2.3 Uchambuzi wa Machapisho ya Ziada

**Muda: saa 5**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kubainisha machapisho ya ziada ya kufundishia somo la Haiba na Michezo

b) Kueleza sifa za machapisho bora ya ziada ya kufundishia na kujifunzia somo la Haiba na Michezo
c) Kutumia machapisho ya ziada katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Kazi za maktaba kuchambua na kuwasilisha ripoti ya machapisho na vitabu vya ziada vinavyofaa kufundishia na kujifunzia somo la Haiba na Michezo kwa shule za Msingi.
b) Majadiliano ya vikundi na uwasilishaji.

**Zana/vifa vya kufundishia/kujifunzia**

a) Machapisho mbalimbali ya elimu ya Haiba na Michezo
b) Vitabu mbalimbali vya ziada kwa somo la Haiba na Michezo
c) Maswali ya uchambuzi yaliyotayarishwa.

**Upimaji**

Insha, majaribio na mkoba wa kazi.

## 2.4 Uchambuzi wa Kiongozi cha Mwalimu

**Muda: Saa 4**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kuchambua kiongozi cha mwalimu kwa somo la Haiba na Michezo
b) Kueleza umuhimu muhtasari wa somo, kitabu cha kiada na kiongozi cha mwalimu kwa somo la Haiba na Michezo

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

Kazi za maktaba, majadiliano ya vikundi vikundi na uwasilishaji.

**Zana/vifa vya kufundishia/kujifunzia**

Nakala za muhtasari, vitabu vya kiada na kiongozi cha mwalimu.

**Upimaji**

Kazi binafsi kuchambua na kuandika ripoti kuhusu uhusiano uliopo kati ya muhtasari wa Somo la Haiba na michezo elimu ya msingi, vitabu mbalimbali vya kiada na kiongozi cha mwalimu.

## 3.0 ZANA ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA

### 3.1 Aina za Zana

**Muda: Saa 4**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kuainisha zana za kufundishia na kujifunzia somo la Haiba na Michezo.
b) Kueleza umuhimu wa kutumia zana katika kufundishia/kujifunzia somo la Haiba na Michezo.
c) Kubainisha mambo ya kuzingatia katika kuchagua na kutumia zana za kufundishia na somo la Haiba na Michezo.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

Majadiliano katika vikundi, maswali na majibu .

Ufundishaji rika

**Zana/vifaa vya kufundishia/kujifunzia**

a) Muhtasari wa somo la Haiba na Michezo shule za msingi.
b) Kiongozi cha mwalimu somo la Haiba na Michezo shule za msingi.
c) Mwongozo wa kutengeneza zana.

**Upimaji**

Maswali ya mafupi, Insha mkoba wa kazi

### 3.2 Upatikanaji wa Zana

**Muda saa 6**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kueleza mbinu za kupata zana za kufundishia/kujifunzia somo la Haiba na Michezo.
b) Kuandaa zana za kufundishia somo la Haiba na Michezo kwa kufaragua na kutengeneza.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Majadiliano kwa vikundi kuainisha zana zinazofaa kwa kuzingatia mada katika kufundisha somo la Haiba na Michezo
b) Kuandaa na kukusanya vifaa au malighafi ya kutengenezea zana za kufundishia somo la Haiba na Michezo
c) Onyesho mbinu la kufaragua na kutengeneza zana za kufundishia na kujifunzia .

**Zana/vifa vya kufundishia/kujifunzia**

a) Muhtasari wa Somo la Haiba na Michezo shule za msingi.
b) Mifano ya zana zinazoweza kufaraguliwa na kutumia kufundishia na kujifunzia somo la Haiba na Michezo.
c) Vifaa vya kutengenezea na kufaragua zana za kufundishia.

**Upimaji**

Kazi mradi, fomu ya uchunguzi na fomu ya ulinganifu wa viwango

## 3.3 Matumizi na utunzaji wa zana za kufundishia na kujifunzia

**Muda saa 6**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kueleza umuhimu wa kutumia zana sahihi na kwa usahihi kufundishia na kujifunzia somo la Haiba na Michezo
b) Kutunza zana za kufundishia na kujifunzia Haiba na Michezo
c) Kueleza mambo ya kuzingatia wakati wa matumizi ya zana

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Onyesho mbinu la matumizi sahihi ya zana katika ufundishaji na ujifunzaji.
b) Majadiliano kwa vikundi kuainisha manufaa na changamoto za kutumia na kutunzia zana za kufundishia na kujifunzia.
c) Onyesho mbinu kuonyesha adhati za kutotumia zana /vifaa vya michezo kwa usahihi

**Zana/vifaa vya kufundishia/kujifunzia**

a) Muhtasari wa somo la Haiba na Michezo shule za msingi.
b) Zana za kufundishia na kujifunzia. Mfano mipira, upinde, mshale na tufe.

**Upimaji**

Insha, Orodha hakiki na Fomu ya ulinganifu wa vitendo.

## 4.0 MAANDALIZI YA UFUNDISHAJI WA SOMO LA HAIBA NA MICHEZO

### 4.1 Uandaaji wa Azimio la Kazi

**Muda saa 6**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kuandaa Azimio la Kazi.
b) Kutumia Azimio la Kazi

**Mbinu za Kufundishia/kujifunzia**

a) Kazi binafsi na kazi za maktaba kuandaa azimio la kazi
b) Onyesho mbinu la kuandaa Azimio la Kazi.

**Vifaa na zana za kujifunzia na kufundishia**

a) Mwongozo wa Ufundishaji na Ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo kwa shule za msingi.
b) Mchoro unaoonyesha mfano wa Azimio la Kazi
c) Muhtasari wa Haiba na Michezo.
d) Vitabu vya rejea, kiada, kiongozi cha mwalimu na moduli

**Upimaji**

Orodha hakiki, fomu ya mlinganisho wa viwango na fomu ya uchunguzi.

## 4.2 Andalio la Somo

**Muda saa: 6**

**Malengo mahsusi**

**Malengo Mahususi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kubainisha vipengele vya andalio la somo.
b) Kubainisha maudhui ya azimio la kazi yanayotakiwa kuingia katika andalio la somo.
c) Kuandaa andalio la somo.
d) Kutumia andalio la somo lililoandaliwa.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Maswali na majibu , bungua bongo, kubainisha vipengele
b) vya andalio la somo na vipengele vya azimio la kazi vinavyotakiwa kuingia katika andalio la somo.
c) Kazi binafsi kuandaa andalio la somo kwa kutumia azimio la kazi
d) Ufundishaji rika

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Andalio la somo la mfano.
b) Azimio la kazi, vitabu vya kiada, ziada na rejea.

**Upimaji**

a) Zoezi na majaribio
b) Orodha hakiki na fomu ya ulinganifu wa viwango.

## 4.3 Uandaaji wa Shajara ya Somo:

**Muda saa: 4**

**Malengo mahususi**

Baada ya kujifunza mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kufafanua vipengele vya shajara ya somo
b) Kubainisha maudhui ya azimio la kazi yanayotakiwa kuingia katika shajara ya somo.
c) Kuandaa shajara ya somo.
d) kutumia shajara ya somo.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Majadiliano ya kikundi kufafanua katika vipengele vya shajara ya somo na kubainisha maudhui ya azimio la kazi yanayotakiwa kuingia katika shajara ya somo.

b) Mjadala kujadili umuhimu wa kuandaa shajara ya somo.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Shajara ya somo ya mfano.
b) Azimio la kazi

**Upimaji**

Zoezi, insha kueleza vipengele na umuhimu wa kuandaa shajara
Orodha hakika na mkoba wa kazi.

## 4.4 Nukuu za Somo

**Muda saa: 6**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kusoma mada hii, mwanachuo aweze:

a) Kubaini vipengele vya kuzingatia wakati wa kuandaa nukuu za somo.
b) Kuandaa nukuu za somo.
c) Kutumia nukuu za zilizoandaliwa.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Usomaji bainifu wa matini ya mada mbalimbali ili kuandaa nukuu.
b) Kazi mradi kuandaa nukuu za somo zinazotosheleza.
c) Kutumia nukuu za somo katika ufundishaji.

**Vifaa na zana za kujifunzia na kufundishia**

Vitabu vya rejea, kiada, ziada, kiongozi cha mwalimu na sampuli za nukuu za somo.

**Upimaji**

a) Fomu ya mlinganisho wa viwango kuhusu uwezo wa kuandika nukuu za somo.
b) Majaribio kuhusu uandaaji wa nukuu za somo.

### 4.5 Ufundishaji wa Mfano

#### 4.5.1 Stadi za uchezaji wa mpira wa miguu

**Muda saa:6**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kupasha mwili joto.
b) Kuanisha stadi za utoaji wa pasi .
c) Kuonyesha stadi za utoaji wa pasi .
d) Kupoza mwili.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Vikundi vidogo vidogo kuonesha mazoezi ya kupasha mwili joto.
b) Kazi za maktaba na onesho mbinu kuonesha utoaji wa pasi mbalimbali

**Vifaa na zana za Kufundishia na kujifunzia**

a) Azimio la kazi.
b) Andalio la somo.
c) Filimbi, mipira na koni.

**Upimaji**

Fomu ya uchunguzi kuhusu uandaaji na ufundishaji wa somo . Orodha hakiki na fomu ya mlinganisho wa vitendo.

**4.5.2 Sheria za Mpira wa Kikapu**

**Muda saa:6**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kuainisha sheria za mpira wa kikapu.
b) Kutafsiri sheria za mpira wa kikapu
c) Kutumia sheria katika uchezaji wa mpira wa kikapu

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

Vikundi vidogo vidogo, kazi za maktaba , majadiliano ya vikundi na uwasilishaji na onyesho mbinu.

**Vifaa na zana za Kufundishia na kujifunzia**

a) Azimio la kazi

b) Andalio la somo
c) Filimbi, mipira na koni

**Upimaji**

Fomu ya uchunguzi kuhusu uandaaji na ufundishaji wa somo . Orodha hakiki na fomu ya mlinganisho wa vitendo

## 5.0 UPIMAJI NA TATHIMINI YA UFUNDISHAJI WA SOMO LA HAIBA NA MICHEZO

### 5.1 Upimaji katika somo la Haiba na Michezo

**Muda saa 7**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kufafanua umuhimu wa upimaji katika somo la Haiba na Michezo.
b) Kubainisha mambo ya kuzingatia katika upimaji wa somo la Haiba na Michezo.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

Maswali na majibu,bungua bongo  na kazi za vikundi kuandaa zana za upimaji wa somo la Haiba na Michezo.

**Zana/vifaa vya kufundishia/kujifunzia**

a) Kiongozi cha mwalimu somo la Haiba na Michezo shule za msingi.
b) Kitabu cha kiada cha somo la Haiba na michezo shule za msingi.
c) Muhtasari wa somo la Haiba na Michezo shule za msingi.
d) Machapisho na maandiko yahusuyo upimaji na tathmini.
e) Mifano mbalimbali ya zana za upimaji.

**Upimaji**

Mkoba wa kazi, kazi binafsi na orodha hakiki.

## 5.2 Zana za Upimaji katika somo la Haiba na Michezo

**Muda: Saa 6**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kubainisha zana zinazokidhi upimaji wa somo la Haiba na Michezo
b) Kutunga maswali ya upimaji kwa kuzingatia jedwali la utahini.
c) Kuandaa mwongozo wa usahishaji.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Kubungua bongo, onesho mbinu, kazi binafsi na majadiliano katika vikundi
b) Majadiliano ya darasa juu ya uhusiano wa maswali yaliyotugwa na jedwali la utahini.
c) Kazi katika vikundi uandaa wa mwongozo wa usahishaji

**Zana/vifaa vya kufundishia/kujifunzia**

a) Mwongozo wa upimaji
b) Andalio la somo.
c) Mfano wa jedwali la utahini.

**Upimaji**

Maswali ya zoezi, Kazi binafsi kuandaa jedwali la utahini, mkoba wa kazi na orodha hakiki.

## 5.3 Tathmini katika somo la Haiba na Michezo

**Muda: Saa 6**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kuainisha mambo muhimu ya kuzingati wakati wa kufanya tathmini

b) Kabainisha aina za tathmini.
c) Kufafanua matumizi ya alama za mazoezi,majaribio na mitihani katika kuboresha ufundishaji wa somo la Haiba na Michezo

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Kazi za vikundi, majadiliano katika vikundi kubainisha mambo yakuzingatia wakati wa kufanya tathmini.
b) Maswali na majibu kufafanua matumizi ya alama za mazoezi,majaribio na mitihani katika somo la Haiba na Michezo

**Zana/vifaa vya kufundishia/kujifunzia**

a) Chati ya nyanja za upimaji na ngazi zake.
b) Aina mbalimbali za maswali na muongozo wa usahihishaji.
c) Mwogozo wa upimaji na tathmini.
d) Kadi za maendeleo ya wanafunzi.

**Upimaji**

a) Zoezi la kutunga maswali ya mtihani na mazoezi kwa kuzingagia nyanja za upimaji na ngazi zake.
b) Zoezi la kusahihisha mitihani na mazoezi kwa kutumia mwongozo wa usahihishaji wa somo.

**Rejea**

Kiganjo, G. and Mwathi, L. (2003). *Physical Education*: A teachers' Guide for Form Three. The Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi.

Ministry of of Education and Culture (2005): *Physical Education Syllabus for Secondary Schools*. Form I – IV. Dar-es-Salaam.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (2005) *Muhtasari wa somo la Haiba na Michezo shule za msingi*, Taasisi ya Elimu Tanzania. Dar-es-salaam.

Wizara ya Elimu na Utamaduni (2003) *Muhtasari wa Mafunzo ya Ualimu ngazi ya Cheti* –Mbinu za kufundishia Stadi za Kazi Tanzania. Taasisi ya Elimu Tanzania. Dar es Salaam.

Wizara ya Elimu na Utamaduni (2003) *Muhtasari wa Elimu kwa Michezo ngazi ya Diplom***a** –Taasisi ya Elimu Tanzania. Dar es Salaam, Tanzania.